{«DateLetterGenerated»}

{«PropertyOwnerName»}
{«MailAddress»}
{«MailCity», «MailState» «MailZip»}

Mpendwa {«PropertyOwnerName»}:

Barua hii ni kukujulisha kwamba mnamo {«LHCOdate»}, Amri ya Kudhibiti Hatari za madini ya Risasi ilitolewa kwa jengo lililoko katika {«PropertyAddress»}. Mnamo {«NONCOVdate»}, Notisi ya Kukosa Utiifu na Amri ya Kuondoka ilitolewa. Amri na notisi zilitolewa kwako kwa sababu jina hili liliorodheshwa kwenye rekodi za mali za kaunti ya {«CountyName»} kama mmiliki wa jengo. Idara ya Afya ya Ohio hivi majuzi ilipokea habari inayoonyesha kuwa unahifadhi hati miliki ya kisheria kwa mali kupitia utwaliwaji au uhamisho. Kifungu cha 3742.38 cha Sheria Iliyorekebishwa kinaeleza kuwa mmiliki wa jengo atashirikiana na Mkurugenzi wa Afya au Bodi ya Afya katika kudhibiti kila hatari ya madini ya risasi iliyobainishwa katika amri hiyo. Kama mmiliki wa jengo la sasa, una jukumu la kufuata amri; kwa hivyo, nakala hii ya Amri ya Kudhibiti Hatari za madini ya Risasi na Ukaguzi wa Hatari ya madini ya Risasi kwa Afya ya Umma inatumwa kwako. Kwa hivyo umeamriwa kudhibiti hatari za madini ya risasi ndani ya siku tisini (90) baada ya kupokea amri hii.

Unahitajika kuchagua njia ya kudhibiti kutoka kwa chaguo zinazowezekana zilizoainishwa katika orodha iliyoambatishwa yenye kichwa cha *"Uteuzi wa Njia ya Udhibiti wa Hatari ya madini ya Risasi."* Fomu hii lazima irudishwe kabla ya kuanza kwa kazi ya kudhibiti hatari ya madini ya risasi kwa {«HDRepresentative»} kupitia faksi au barua pepe kwa {«HDphone»} au {«HDemail»}.

Kama mmiliki, lazima uchukue hatua za kudhibiti hatari za madini ya risasi zilizoorodheshwa katika amri hii kulingana na Sura ya 3742. ya Sheria Iliyorekebishwa na Sura za 3701-30 na 3701-32 za Sheria ya Utawala ya Ohio. Kwa mujibu wa kanuni ya 3701-32-03(A)(14) ya Sheria ya Utawala ya Ohio, kazi ya kudhibiti hatari ya madini ya risasi lazima ifanywe na mtu aliyepewa leseni katika Ohio kama mkandarasi wa kupunguza madini ya risasi.

Wakati wa kukamilisha kazi ya kudhibiti hatari ya madini ya risasi, lazima jengo lipite uchunguzi wa kibali. Uchunguzi wa kibali lazima ufanywe na mkaguzi wa hatari ya madini ya risasi au mkaguzi mkuu aliyepewa leseni katika Ohio. Ikiwa vidhibiti vya muda (muda mfupi) vinatumika kudhibiti hatari lazima uwasilishe "Mpango wa Ufuatiliaji na Matengenezo Unaoendelea (Ongoing Monitoring and Maintenance (OMM))." Lazima utume nakala ya ripoti ya uchunguzi wa kibali na mpango wa OMM, ikiwa inafaa, kwa {«HDRepresentative»} kupitia faksi au barua pepe kwa nambari ya faksi au anwani ya barua pepe iliyoorodheshwa hapo juu.

Mara tu inapobainishwa kuwa hatari za risasi zinadhibitiwa vya kutosha, Idara ya Afya ya Ohio itatoa na kukutumia "Notisi ya Utiifu" ikiondoa amri ya kudhibiti hatari za risasi. Hadi wakati huo, jengo linabaki chini ya amri hii ya kudhibiti.

Kushindwa kutii amri hii kunaweza kusababisha amri inayokataza matumizi ya jengo kama kitengo cha makazi, kituo cha huduma ya matunzo ya watoto au shule na kubandikwa kwa bango kwenye jengo linaloonya umma kwamba jengo hilo sio salama kwa makazi ya binadamu.

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu amri hii, tafadhali pigia simu {«HDRepresentative»} kupitia {«HDphone»}.

Kwa Uaminifu,

{«HDRepresentativeName»}
{«HDRepresentativeTitle»}
{«HDName»}